



independence INC

YOU'RE THE EXPERT ON YOU!

We're here to help

Kuwahudumia watu wa umri wote wenye ulemavu wa aina yoyote

Independence, Inc. • www.independenceinc.org

Huduma za Msingi Kaunti za Wy na Jo Wy Co

Mawasiliano: LaNeece Jardon, Meneja wa Huduma za Msingi, ljardon@independenceinc.org

Tumepana huduma zetu kutoka Lawrence hadi Jiji la Kansas, eneo la KS! Huduma zetu za msingi zinazopatikana katika Kaunti za Wyandotte na Johnson ni pamoja na:

Utetezi: Huduma za utetezi zinaweza kukusaidia kuelewa sheria zinazokulinda na kushughulikia mizozo migumu na hali nyingine kwa ujasiri kwa matokeo mazuri kwa wote.

Taarifa na Rufaa: I&R ni huduma muhimu, inayokuunganisha na mipango, huduma, bidhaa na fursa za jumuiya na jimbo zima ambazo zinaweza kumnufaisha mtu mwenye ulemavu.

Mafunzo ya Stadi za Maisha ya Kujitegemea (IL): Kusaidia kuboresha uhuru na uwezo wa kuishi maisha yenyе utendaji, yenyе tija katika nyumba na jumuiya unayochagua.

Usaidizi wa Rika: Usaidizi wa Rika unaweza kumsaidia mtu aliye na ulemavu kushughulikia na hali za maisha, mifumo, urafiki na uhusiano mwagine na jumuiya kwa ujumla, na pia kusaidia katika kujipatia ujasiri na kufanya marafiki wazuri.

Maisha ya Kujitegemea: Kutoa huduma za kumsaidia mtu mwenye ulemavu kuondoka katika nyumba au taasisi ya uuguzi na kurudi kwenye jumuiya na kwenda kwenye makazi ya chaguo lake.

Ushauri wa Mpito wa Vijana: Kwa vijana na watu wazima vijana wanaotamani kubadilika kutoka shule ya sekondari au ajira ya muda, kwenda ajira ya kudumu, mafunzo, shule ya ufundi au chuo, ikiwemo usaidizi wa IEP, mafunzo ya stadi za kujitegemea za maisha, kutambua vipaji na mapendeleo na kuchukua hatua inayofuata kuelekea utu uzima.

Huduma za Usimamizi wa Fedha

Mawasiliano: Alisa Snyder, Meneja wa Mshahara wa FMS asnyder@independenceinc.org | 785-841-0333 X 120

Huduma za Usimamizi wa Fedha (FMS) zinapatikana kwa watu wanaostahiki wenyе ulemavu wanaotaka kuelekeza huduma zao za kibinasi chini ya Mpango wa Msamaha wa HCBS wa Kansas Medicaid. Wewe, kama mwajiri, utaaajiri, kufundisha, na kusimamia Mfanyakazi wako wa Huduma ya Utunzaji wa Kibinasi (PCSW), wakati tunashughulikia usimamizi wa kifedha/mshahara kwa ajili yako na mfanyakazi wako.

Huduma zinajumuisha, maandalizi ya mishahara, kuandikisha taarifa za mishahara inayohusika, kodi za W-2, bima ya ukosefu wa ajira na bima ya mshahara wa mfanyakazi.

Mtando wa Mpito wa Vijana wa Kansas:

Mawasiliano: Amy Ballinger, Meneja wa Mpango wa KYTN, aballinger@independenceinc.org | 785-371-1646

Tunafanya kazi ndani ya Mtando wa Mpito wa Vijana wa Kansas kutoa Huduma za Mpito wa Vijana zilizopanuliwa ndani ya Kaunti ya Wyandotte ili kusaidia malengo ya maisha ya kujitegemea na ajira ya vijana wenyе ulemavu. Tunafanya kazi na vijana wenyе umri wa miaka 10 kwenda juu ili kusaidia kutambua na kuimarisha mapendeleo na vipaji, kukuza malengo ya baadaye na kutoa fursa za ushiriki wa shule na jumuuya, usaizidi wa marika na hatimaye fursa za ufundi, elimu ya juu au mafunzo ya kiufundi. Tunafanya hivyo kupitia:

- mafunzo ya darasani ya
- kikundi/warsha IEP au usaizidi na
- utetezi wa 504
 - stadi za maisha na mafunzo ya stadi za maisha ya
 - kujitegemea kama vile jinsi ya kusimamia pesa
 - utatuvi wa migorogo
 - stadi za kujitegemea na ujuzi wa kujitetea kusafisha/kupanga na usimamizi wa wakati
- Maendeleo ya stadi za ufundi kama
 - vile kutafuta kazi
 - kuandika wasifukazi/mahojiano
 - stadi za ishara za mwili/mawasiliano, na mengi zaidi!

Mipango ya KAZI na HATUA ya KANSAS

Mawasiliano: Jennifer Moore, Meneja wa Mpango wa KAZI, jmoore@independenceinc.org | 785--371-0888

Mpango wa Kansas wa Nafasi za Kazi Kuwatunza Wakazi wa Kansas (KAZI) ni sehemu ya mpango wa Kufanya Kazi kwa Afya na hutoa huduma mbalimbali kwa wale wanaohitaji usaizidi wa ziada. Umeundwa kusaidia watu wanaofanya kazi wenyе ulemavu wenyе umri wa miaka 16 na zaidi, kufuutilia malengo yao ya ajira bila kupoteza bima ya huduma za afya. Kupitia mpango wa KAZI, Mshauri wa Maisha ya Kujitegemea atasaidia kukuongoza kupitia mchakato wa ajira, kusikiliza malengo yako na kutoa usaizidi ili kusaidia kufikia malengo hayo.

Usaidizi na Mafunzo ya Kuwaajiri Watu kwa Mafanikio (STEPS) ni mpango ambaPo watu wenyе ulemavu na/au matatizo fulani ya afya ya tabia wanaweza kutafuta njia ya kuajiriwa bila kupoteza mafao ya Hifadhi ya Jamii au bima ya matibabu. Kwa wale wanaostahiki, huduma zinaweza kujumuisha: Huduma za Kabla ya Mafunzo ya Kitaaluma, Mafunzo ya Stadi za Maisha ya Kujitegemea, Huduma za Msaidizi wa Binafsi, Usafiri, Ajira Zinazosaidiwa, Teknolojia ya Kusaidia na Uratibu wa Huduma za Jumuiya.

